RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO NA UJENZI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015
SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ilioundwa kwa Mujibu wa Kanuni ya 106(d) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012. Majukumu ya Kamati yameelezwa katika Kanuni ya 111 ya kanuni hizo ambapo majukumu ya msingi ya Kamati ni kama yafuatayo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

WAJUMBE WA KAMATI

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ina jumla ya Wajumbe Saba, wakisaidiwa kwa karibu na Makatibu wawili, Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa — Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu — Mjumbe
4. Mhe. Marina Joel Thomas — Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe

6. Mhe. Salma Mohammed Ali Mjumbe

7. Mhe. Mohammed Haji Khalid Mjumbe

8. Ndg. Maryam Rashid Ali Katibu

9. Ndg. Saad Othman Saad Katibu

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ina jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji katika Wizara mbili nazo ni:-

1. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, na

2. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka 2014/2015 ilifanya kazi kwa muda wa Wiki nne.

- Wiki mbili za mzunguko mwanzo: 8/12/2014 - 19/12/2014 (Pemba)

- Wiki mbili za mzunguko wa Pili: 02/02/2015 – 13/02/2015 (Unguja)

Katika mizunguko hiyo Kamati ilipata nafasi ya kukagua, kutembela na kuhoji kuhusiana na masuala mbali mbali yanayohusu utekelezaji wa Shughuli mbali mbali za Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Miongoni mwa Kazi zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi hicho ni kama zifuatazo:

I. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kazi za kila siku za Wizara.

II. Kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015

III. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, na

IV. Kutembelea taasisi mbali mbali za Wizara husika kwa lengo kujifunza.

SEHEMU YA PILI

WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imeundwa na idara na Taasisi zifuatazo.

i. Idara ya Mipango
ii. Idara ya Utumishi na Uendeshaji
iii. Idara ya Ardhi na Usajili
iv. Idara ya Upimaji na Ramani
v. Idara ya Mipango Miji na Vijiji
vi. Idara ya nyumba na Maendeleo ya Makaazi

vii. Idara ya Nishati na Madini
viii. Idara ya Ujenzi
ix. Mahakama ya Ardhi
x. Msajili wa Ardhi
xi. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe
xii. Mamlaka ya Maji (ZAWA)
xiii. Shirika la Umeme (ZECO)

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Idara hii ina jukumu la kusimamia masuala yote yanayohusu Rasilimali watu katika Wizara hii ambayo inajumuisha, mishahara, mafao, uajiri nk. Kimsingi Idara hii ndio inayotekeleza majukumu ya kusimamia Wizara nzima. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Idara hii imeendelea kutekeleza kazi zake kwa ufanisi licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali

CHANGAMOTO

1. Ufinyu wa Bajeti; Idara hii licha ya kubeba jukumu la uendeshaji wa Wizara nzima lakini bajeti inayotengewa ni chache hali inayopelekea baadhi ya shughuli kutokutekelezwa.

MSAJILI WA ARDHI, IDARA YA ARDHI NA USAJILI, IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI, IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI (LAND HOUSE)

Afisi ya Msajli wa Ardhi, Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji (Land House) ni Idara zinazoshughulikia masuala ya Ardhi na hufanya kazi zao kwa mashirikiano ya karibu sana katika kusimamia masuala ya Ardhi Zanzibar.

Afisi ya Msajili wa Ardhi ina jukumu la kufanya utambuzi na kusajili Ardhi Zanzibar chini ya Sheria no 10 ya 1990, Afisi hii imeendelea na kazi ya kusajili Ardhi kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi ambapo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imeendelea na usajili wa Ardhi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Aidha Afisi imeendelea na zoezi la utambuzi wa Ardhi pamoja na kuendelea kutoa elimu ya usajili wa Ardhi kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, semina, vipeperushi na majarida, licha ya kuendelea na kazi hizo Afisi bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali.

IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI

Idara ya Mipango Miji na Vijiji ina jukumu la kupanga matumizi ya Ardhi pamoja na kuendeleza mji wa Zanzibar.

CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI IDARA ZINAZOSIMAMIA ARDHI

1. Uchache wa Wafanyakazi; kamati imebaini kuwa Afisi ya msajili wa Ardhi ina uhaba wa wafanyakazi hali inayopelekea zoezi hilo kufanyika kwa kasi ndogo, ambapo kamati ilielezwa kuwa Afisi ina wafanyakazi 3 ambao hawatoshelezi ukizingatia ukubwa wa kazi yenyewe.

2. Kutokuwepo kwa fedha ya uhakika kwa ajili ya kuendeleza usajili wa Ardhi hasa ukizingatia kwamba mradi wa Smole unatarajia kumaliza muda wake.

3. Ukosefu wa ujuzi wa kutosha wa masuala ya utambuzi na usajili wa Ardhi kwa watendaji wa Afisi

4. Uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya usajili wa Ardhi hali inayopelekea zoezi la usajili kutokuenda kwa haraka.

5. Kukosekana kwa mashirikiano baina ya idara ya Mipango Miji na Vijiji, Manispaa na Halmashauri za Miji hali inayopelekea kutokuwepo kwa mawasiliano mazuri wakati wa utoaji wa vibali vya ujenzi na kusababisha ujenzi usiozingatia mipango ya mji.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI

a) Kamati inaishauri Wizara kuwapatia afisi ya msajili wa Ardhi wafanyakazi wa kutosha katika bajeti ya mwaka 2015/2016 ili kazi ya usajili wa Ardhi iweze kufanyika kwa ufanisi

b) Kamati imeiagiza Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kubuni mradi mwengine kwa lengo la kupata fedha ya kuendeleza shughuli za Usajili wa Ardhi.

c) Kamati imeitaka Wizara kuwapatia Watendaji wa Afisi ya Msajili wa Ardhi mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya masuala ya usajili wa Ardhi lil watekeleze kazi zao kwa ufanisi utakaojumuisha ziara za kimafunzo katika nchi jirani ambazo wamefanikiwa katika zoezi la kusajili Ardhi kama vile, Mauritius, Rwanda nk.

d) Kamati imeshauri Afisi ya Msajili wa Ardhi kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya masuala ya usajili na utambuzi wa Ardhi na umuhimu wake katika maendeleo ya nchi yao.

e) Kamati inazishauri Idara zinazoshughulikia masuala ya Ardhi kufanya kazi kwa mashirikiano na taasisi nyengine kama vile Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Mamlaka ya vitega uchumi (ZIPA) ili kuhakikisha kuwa kazi zao zinafanyika kwa ufanisi.

MAHAKAMA YA ARDHI

Mahakama ya Ardhi ni miongoni mwa Idara zilizo chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, maji na Nishati ambapo jukumu la msingi la taasisi hiyo ni kusikiliza madai yanayohusiana na Ardhi kwa lengo la kutoa haki. Taasisi hii imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na inakabiliwa na changamoto zifuatazo.

1. Uhaba wa majengo kwa ajili ya mahakama; Kamati imebaini kuwa suala la uhaba wa majengo bado ni tatizo kubwa kwa Mahakama ya Ardhi hali inayopelekea kufanya kazi zao katika mazingira magumu, sambamba na hilo mahakama hadi hivi leo imeshindwa

kukamilisha ujenzi wa ofisi ya mahakama yake unaoendelea kujengwa Koani na Gamba kutokana na kukosa fedha za kumalizia ujenzi huo.

2. Uchache wa mahakimu; mahakama ya Ardhi inakabiliwa na uhaba wa mahakimu kwa ajili ya kusikiliza kesi za ardhi hali inayopelekea uzorotaji wa usikilizwaji wa kesi na madai ya ardhi.
3. Ukosefu wa usafiri; tatizo la usafiri nalo limekuwa bado ni tatizo la muda mrefu kwa taasisi nyingi zilizo chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ikiwemo taasisi hii ya mahakama ya Ardhi hali inayozorotesha ufanisi wa kazi za kila siku za Mahakama.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI

a) Kamati imeishauri Wizara kuhakikisha inaipatia mahakama ya Ardhi fedha kwa ajili ya kumalizia na kukamilisha ujenzi wa majengo yake ya mahakama ya Koani na Gamba katika bajeti ya mwaka 2015/2016.

b) Kamati imeishauri Wizara kuwapatia mahakama ya ardhi mahakimu wa kutosha kwa ajili ya kuhakikisha kesi zinasiklizwa kwa haraka na kuondosha mrundikano wa kesi.

c) Kamati inaishauri Wizara kuchukua hatua za dharura ili kuhakikisha kuwa mahakama inapatia usafiri kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi zao.

MAMALAKA YA MAJI (ZAWA)

Mamlaka ya Maji (ZAWA) ina jukumu la kudhibiti, kusimamia na kulinda vianzio vya maji, kutoa na kusambaza maji pamoja na kusimamia uzalishaji wa maji Zanzibar, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka imeendelea na utekelezaji wa kazi zake kwa kusimamia na kuendeleza mipango mbali mbali ya usambazaji wa maji mijini na vijijini, katika kutekeleza mipango hiyo miradi mbali mbali imeendelezwa ikiwemo miradi ya usambazaji maji na usafi wa mazingira, mradi wa kuimarisha miundombini ya maji nk. Katika kutekeleza majukumu yake mamlaka inakabiliwa na changamoto zifuatazo.

CHANGAMOTO

1. Ongezeko la Mahitaji; Kamati imeelezwa kuwa miongoni mwa changamoto zilizopo katika mamlaka ya maji ni kuongezeka kwa mahitaji kunakosababishwa na ukuaji wa maendeleo katika nchi yetu, hivyo kutokana na ongezeko hilo mahitaji ya maji yamekuwa ni makubwa ukilinganisha na uzalishaji wenyewe.

2. Uchakavu wa miundombinu ya Maji; Kamati imebaini kuwa miundombinu iliyopo ya maji ni chakavu sana kwani yamejengwa miaka mingi iliyopita ambayo ni mtandao wa mabomba ya udongo (Asbestos cement pipes), aidha mtandao huo ulijengwa kuhudumia idadi ya watu wasiozidi 50,000 kwa mji wa Unguja, hivyo basi mtandao huo haukidhi mahitaji ya wakati huu hali inayopelekea maji mengi kupotea njiani kutokana na ubovu wa mabomba hayo.

3. Kuwepo kwa mabadiliko ya tabia nchi; mabadiliko ya tabia nchi yanayotokea ulimwenguni nayo pia yamepelekea kupungua kwa rasilimali ya maji ardhini kutokana na kupatikana kwa kiwango kidogo cha mvua au wakati mwengine kukosekana kabisa katika muda unaotarajiwa, hivyo hali ya uzalishaji maji imekuwa ikipungua kutokana na mabadilko hayo.

4. Kutokuwepo kwa mita za maji kwa watumiaji; Mamlaka pia imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa mita za maji kwa watumiaji hali inayopelekea wananchi kutumia maji bila ya kuwa na kipimo cha matumizi halisi ya maji hayo na kupelekea kuwa na matumizi makubwa ya maji yasio na ulazima na hatimae kulipia ada ndogo ya maji (flate rate)

5. Uvamizi wa maji chumvi katika vianzio vya Maji; kumekuwepo na mabadiliko ya ubora wa maji kwa kujitokeza viashiria vya chumvi katika mapango na visima vingi hususan vilivyo karibu na ukanda wa bahari, aidha uchimbaji holela wa visima nao umechangia kuwepo kwa uharibifu huo.
6. Ungezeko la ujenzi wa nyumba usiofuata taratibu za mipango miji; kuongezeka kwa ujenzi holela wa makaazi kusikofuata utaratibu kunasababisha kuvamiwa kwa miundombinu ya maji na kufanyika uharabifu na kusababisha usumbufu mkubwa wakati wa matengenezo na matunzo ya vianzio hivyo.

7. Ukomo wa Makadirio ya Bajeti; Kukosekana kwa fedha za kutosha kwenye Bajeti ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayotokana na ukomo mdogo wa Bajeti hupelekea Mamlaka kushindwa kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya huduma ya maji.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI

a) Kamati inaishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa inafunga mita za maji kwa wateja kupitia bajeti yake ya ndani kwa lengo la kuwashawishi na washirika wa maendaleo kuwasaidia katika kununua na kufunga mita hizo

b) Kamati inaishauri Mamlaka kuwa na mashirikiano na taasisi nyengine zinazohusika na matumizi bora ya Ardhi kama vile Idara ya Mipango miji na Vijij, halmashauri za Wilaya na Manispaa na taasisi zinazotoa huduma za kijamii ili kufanya kazi kwa pamoja katika kuondosha tatizo la ujenzi holela na uvamizi wa vianzio vya maji.

c) Kamati inaishauri Mamlaka kuendeleza utojai wa elimu kwa wananchi juu ya uhifadhi wa vianzio vya maji pamoja na kuwashajihisha kuchangia huduma za maji il mamlaka iweze kutoa huduma zilizo bora zaidi

d) Kamati inaiagiza Wizara kuangalia uwezekano wa Mamlaka kupandisha ada ya huduma ya maji kutoka Shilingi 4000 hadi elfu 12000 ili Mamlaka iweze kujiendesha kibiashara.

e) kamati inaendelea kuishauri Mamlaka kulipa kipaumbele zaidi suala la kubadilisha miundombinu ya Maji kwa kuondoa mabomba chakavu na kuweka mabomba yanayokidhi hali ya sasa ili kuepuka upotevu wa rasilimali ya maji
f) Kamati inaishauri Mamlaka kutafuta utaratibu wa kuongeza vianzio vya Maji unguja na Pemba ili viweze kuendana na kuwiana na mahitaji kwa wakati husika kupitia miradi ya Maendeleo.

g) Kamati inaiagiza Wizara kuhakikisha kuwa miradi iliyomalizika ya Lot 2 kwa upande wa vijijini na Lot 3 kwa upande wa mijini kwa Pemba inafanyiwa majaribio kabla ya muda wa majaribio wa mwaka mmoja haujamalizika ambapo imebakia miezi minne tu.

h) Kamati inaishauri Mamlaka wakati wa uwekaji wa miundombinu ya maji ijitahidi kutenganisha baina ya miundombinu ya maji safi na ile ya maji machafu ili kuepusha uwezekano wa kuchanganyika wakati itakapotokezea hitilafu yoyote.

SHIRIKA LA UMEME (ZECO)

Shirika la umeme Zanzibar lina jukumu la kusambaza umeme katika visiwa vya Unguja na Pemba, ambapo umeme huo ZECO inaununua kutoka Shirika la umeme Tanzania (TANESCO), Katika mwaka wa fedha 2014/2015 shirika la umeme limeendelea na shughuli za usambazaji umeme mijini na Vjijini kwa mafanikio licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali.

CHANGAMOTO.

1. **Deni la ZECO wanalodaiwa na TANESCO;**

Miongoni mwa changamoto kubwa inayolikabili Shirika la umeme Zanzibar ni kuwepo kwa deni kubwa wanalodaiwa na TANESCO linalotokana na bili za ununuzi umeme za muda mrefu ambapo hadi kufikia Disemba 2014 shirika lilikuwa linadaiwa bilioni 49.5

Kamati ilielezwa kuwa ukuaji wa deni hilo unasababishwa na ZECO kukosa uwezo wa kulipia bili zake za kila mwezi kwa ukamilifu, isipokuwa kwa baadhi ya miezi, hali inaporuhusu Shirika huwa inalipa bili yake kwa ukamilifu, na kamati ilipewa taarifa kuwa shirika kwa kawaida huwa inalipa sehemu tu ya bili yake ya kila mwezi kwa mujibu wa uwezo wake wa mapato inayokusanya kutokana na uuzaji wa umeme na hivyo kupelekea mkusanyiko wa bakaa za madeni katika kila mwezi ambapo shirika hushindwa kulipa.

Sababu zinazopeleka kuongezeka kwa Deni.

- **Uwezo wa kufanya malipo.**
  Pamoja na kujiwekea na kutekeleza mikakati ya kulipa Ankara za matumizi ya umeme ya kila mwezi kwa ukamilifu sambamba na malipo ya kila mwezi kwa lengo la kupunguza limbikizo la deni la nyuma , Shirika la umeme limekuwa linakabiliwa na uwezo mdogo wa kumudu kulipa malipo hayo.

- **Kupanda kwa bei ya Umeme kutoka TANESCO.**

Shirika la umeme TANESCO limepandisha bei ya kuuzia umeme kwa asilimia 50 mnamo mwezi wa Januari 2014, ambapo ZECO inaendelea kutumia bei ile ile iliyokuwa ikiwatoza wateja wake kabla ya ongezeko hilo la bei ya Tanesco.

- **Taasisi za Serikali (SMT na SMZ) zisizolipa Ankara na madeni ya Umeme.**

  Baadhi ya Taasisi za Serikali ndio wateja wenye madeni makubwa kwa shirika la umeme ambapo madeni hayo yanatokana na malimbikizo ya madeni, Kutoka Disemba 2013 hadi Septemba 2014 deni la julma la taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutoka TZS 17.6 bilioni hadi kufikia 21.2 bilioni, na kwa upande wa Taasisi za Muungano kutoka TZS 0.93 bilioni hadi kufikia 1.12 bilioni.

- **kukosekana kwa mfuko wa usambazaji umeme vijijni.**

  Shirika la umeme limekuwa likitumia fedha zake katika kugharamia usambazaji wa umeme vijijini jambo ambalo kiutaratibu gharama hizi zilitakiwa ziingizwe kwenye bei ya kuuzia umeme au zitolewe moja kwa moja na mfuko wa Serikali au kutumia wakala wa Serikali wa ajili hiyo.

- **Kutofautiana katika Hesabu za Bei**

  Baada ya malalamiko ya bei ya umeme inayouziwa ZECO kutoka TANESCO hatimae ilifikiwa makubaliano kuwa bei ya umeme kwa ZECO iwe ni Tsh 3 pamoja na punguzo la asilimia 31 katika bei hiyo, hata hivyo ZECO kwa upande wake imekuwa likitafautiana na TANESCO katika mahesabu ya kila mwezi zilizopelekea deni hilo kutokana na hoja ambazo Shirika la umeme inaona ni lazima kuzingatiwa, hoja zenyewe ni kama zifuatazo:-

  - Kutoondoa asilimia 31 ya Bei ya umeme ambayo ni punguzo lililotokana na makubaliano. Asilimia hiyo ni sawa na wastani wa **TZS 1,681,882,990.00** kwa mwezi.

  - Tozo ya REA YA asilimia 3 ya Ankara ya mwezi ambayo Zeco inaamini kuwa sio sahihi kulipia tozo hiyo kwa vile inahusiana na usambazaji wa umeme katika vijiji vya Tanzania bara pekee. Tozo hiyo ni sawa na wastani wa **TZS 160,745,970.00** kwa mwezi.

  - Tozo ya EWURA ya asilimia 1 ya Ankara ya mwezi ambayo Zeco inaamini sio sahihi kuhusishwa nayo, tozo hiyo ni sawa na wastani wa **TZS 53,254,290.00** kwa mwezi.

  - Bei kubwa ya kVA (bei hii ni kubwa sana ukilinganisha na bei wanazotozwa wateja waliopo Tanzania Bara. Zeco inatozwa bei ya TZS 16,550.00 kwa uniti moja kVA sawa na mtumiaji wa mwisho walioko

Tanzania bara, kwa vile Zeco sio wateja wa mwisho ambayo nayo pia inasambaza umeme kwa wateja wake ambao ndio watumiaji wa mwisho, hivyo hali hii huifanya Zeco kubeba pamoja na gharama za usambazaji.

MAKUBALIANO YA ULIPAJI WA DENI KWA TANESCO

Kutokana na ukubwa wa deni Kamati ilipokea taarifa kuwa mashirika mawili haya (ZECO na TANESCO) yakutane pamoja na kufikia makubaliano yafuatayo.

i. ZECO kulipa deni la umeme ambalo limekubaliwa kwa utaratibu kuwa TZS 18 bilioni zitalipwa na Serikali ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ya SMT.

ii. Shilingi bilioni 12 ambazo Zeco inazidai taasisi za Serikali zitalipwa na SMZ kwa kiwango cha Shilingi bilioni 1 kila mwezi.

iii. Zeco itakuwa inalipa Ankara yake kila mwezi kwa ukamilifu kuanzia mwezi Januari 2014.

iv. Kuanzia mwezi Februari 2014 Zeco itakuwa inalipa sambamba na bili ya matumizi ya kila mwezi kwa ukamilifu, ambayo ni shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kupunguza limbikizo la deni.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU DENI LA ZECO KWA TANESCO

a) Kamati inaiagiza Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kusimamia ulipwaji wa Deni la shilingi bilioni 18 kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ya SMT kama ambavyo wamekubaliana.

b) Kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulipa deni la taasisi zake ambalo ni shilingi bilioni 12 kwa utaratibu wa shilingi bilioni 1 kwa mwezi ili shirika liweze kujiendesha kwa faida .

c) Kamati inaishauri Shirika la Umeme ZECO kulipia ankara yake ya bili ya umeme kila mwezi ili kupunguza mrundikano wa madeni ambayo baade inakuwa ni vigumu kuyalipa.

WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeundwa na Idara na Taasisi zifuatazo.

I. Ofisi kuu Pemba
II. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

III. Idara ya Utumishi na Uendeshaji
IV. Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara
V. Idara ya Usafiri na Leseni
VI. Idara ya Mawasiliano
VII. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar
VIII. Mamlaka ya Usafiri Baharini
IX. Shirika la Bandari
X. Shirika la Meli na Uwakala.

IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA (UUB) PEMBA

Idara hii ina jukumu la kusimamia, kujenga na kutunza barabara zote za Pemba. Idara hii kwa upande wa pemba katika mwaka wa fedha 2014/2015 imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, changamoto hizo ni kama zifuatazo.

CHANGAMOTO

1. Kuchelewa kwa fedha za fidia za vipando na nyumba zinazohitajika kuwalipa wakulima 284 kutoka Ole hadi Vitongoji walioathirika wakati ujenzi wa barabara hiyo.

2. Baadhi ya maeneo kwenye barabara ya Ole Kengeja kuna mabomba ya maji na nguzo za umeme vyote ambavyo vyote hivyo vinasababisha usumbufu wa ujenzi wa bara bara.

3. Uhaba wa vitendea kazi kama vile zana nzito na gari za kufanyia kazi na usimamizi.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI.

a) Kamati inaiomba Serikali ichukue deni la ujenzi wa barabara tatu Pemba na kulipeleka katika Taasisi zake za kifedha ili lipunguze kiwango cha riba kutoka asilimia 20 hadi asilimia 5 ili kupunguza hasara kwa kulipa deni hilo ambalo huwaangukia wananchi wanaolipa kodi.
b) Kamati inaishauri Serikali kuwa na akaunti maalum ambayo itasaidia kulipia fidia ya vipando na nyumba kwa miradi ya Serikali na Wafadhili ambao ndani ya miradi yao hamna kifungu cha kulipia fidia.
c) Kamati inaishauri Serikali kupitia madeni ya Wizara ya Miundombinu inayotokana na miradi mbali mbali iliyofanyika ambayo haijalipwa kwa muda mrefu kwa lengo la kulipa.

d) Kamati inaiomba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kusimamia mapendekezo juu ya mikakati wa kuunusuru mradi wa Barabara tatu za Pemba yaliyofanyika Pangani Pemba katika ziara zake za kikazi. Katika majadiliano hayo maazimio ya msingi yalifikiwa ambapo pamoja na kutolipwa deni la sasa la USD 2.5 milioni na TZS 500 milioni kutokana na kazi inayoendelea, na deni la zamani (Lot 2A) la USD 1.7 milioni, Kampuni ya MECCO iko tayari kukamilisha kazi yote iliyobaki iwapo Serikali itawalipa deni la zamani tu la USD 1.7 milioni si zaidi ya tarehe 31 Januari 2014.

SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA

Shirika la meli na uwakala lina jukumu la kuendesha meli zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na kutoa huduma za uwakala wa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar, katika mwaka wa fedha 2014/2015 shirika limeendelea na utekelezaji wa majukumu yake hata hivyo changamoto mbali mbali bado zimekuwa zikilikabili shirika, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo.

Kamati iliarifiwa kwamba meli ya Serikali inayoendelea kujengwa nchini korea imefikia hatua nzuri ambapo hadi mwezi Februari ilikuwa inashushwa kwenye maji (dry docking) kwa ajili ya kumalizia matengenezo madogo madogo. Hata hivyo taarifa kamili ya meli itatolewa na Serikali.

CHANGAMOTO

1. Uchakavu wa Meli za Shirika: Shirika la meli na uwakala kwa sasa limekuwa likiendesha meli mbili ambazo ni meli ya Mv Maendeleo inayopekea abiria na MT Ukombozi inayopakia mafuta, hata hivyo meli hizo ni chakavu na kongwe sana hivyo kupelekea changamoto katika uendeshaji wake kutokana na gharama kubwa za kuzifanyia matengenezo wa mara kwa mara.

2. Ukosefu wa hatimiliki ya Jengo la Shirika: Shirika la meli na uwakala linakabiliwa na tatizo la kukosa hatimiliki ya afisi yao jambo ambalo linawanyiwa fursa ya kulitumia jengo hilo kama ni security wanapotaka kupata mkopo katika mabenki ya fedha

MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI

a) Kamati inaishauri Shirika la meli kuiuza meli ya MT Ukombozi ili inunuliwe meli mpya ya mafuta kama ambavyo imenunuliwa meli mpya ya abiria ambayo inatarajiwa kumalizika hivi karibuni.

b) Kamati inaishauri Wizara kulisaidia Shirika ili kuhakikisha kuwa wanapatiwa hatimiliki ya jengo lao la Ofisi ambayo itawasaidia kuitumia kama ni security wanapoomba mikopo katika mabenki ya fedha.

SHIRIKA LA BANDARI

Shirika la bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa abiria na bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini, vilie vile Shirika lina wajibu wa kuhifadhi mizigo na utunzaji wake katika Bandari. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika limeendelea na kazi zake licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

CHANGAMOTO

1. Mrundikano wa makontena bandarini: Kamati imebaini kuwa mrundikano wa makontena bandarini ni tatizo la muda mrefu linaloikabili Shirika la Bandari hali ambayo inazorotesha shughuli zao za uingizaji wa makontena mapya.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI.

a) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa eneo la malindi ambalo lImekusudiwa kuwekwa makontena baada ya kuhamishwa kutoka bwawani linapatikana ili kupunguza mrundikano wa makontena katika eneo la Bandari.

b) Kamati inalishauri Shirika kutafuta na kufunga machine za kisasa za upekuzi katika jengo la abiria (Terminal) kwa ajili ya kupekuwa abiria na mizigo kwani utaratibu wa upekuzi uliopo kwa sasa ni wa kienyeji zaidi

c) Kamati inaishauri Serikali kulishirikisha Shirika kwa karibu zaidi juu ya mradi wa ujenzi wa Bandari mpya ya mpiga Duri kwa vile wao ndio watakaokuwa wasimamizi wa Bandari hiyo.

d) Kamati imelishauri Shirika la Bandari kuhakikisha kuwa maeneo ya jengo la Abiria (terminal) inatunzwa na kuwekwa katika hali ya usafi muda wote, hivyo Shirika lisimamie watendaji wake ili kuhakikisha kuwa kila wakati watu wa usafi wanasafisha jengo hilo ili libaki na haiba nzuri.

e) Kamati inaendelea kulishauri Shirika kuondoa muhali kwa wafanyabiashara wanaochelewa kuondoa makontena yao kwa kuwachukulia hatua za kisheria ili kupunguza msongamano wa makontena bandarini.

SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR TAWI LA PEMBA
CHANGAMOTO

1. Ukosefu wa kazi za upakiaji na uteremshaji wa mizigo.

2. Uchakavu wa vifaa vilivyopo kwa ajili ya uhudumiaji wa mizigo.

3. Kutotumika ipasavyo kwa bandari kutokana na uchache wa mizigo.

4. Bandari zote zinahitaji maboresho ili ziweze kukidhi mahitaji ya ufungaji wa vyombo vinavyoingia bandarini na uhifadhi wa mizigo.

5. Ukosefu wa uzio katika Bandari pamoja na uvamizi wa maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya Bandari.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI.

a) Kamati imeishauri Shirika la Bandari kutumia bandari yake kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya karafuu moja kwa moja mpaka nchi zinazohusika badala ya utaratibu wa sasa mzigo upelekwe Unguja na kufanyiwa repacking ambapo ni gharama mara mbili ya usafirishaji.

b) Kamati imelitaka Shirika la Bandari kuzungumza na mwekezaji anaetaka kuendeleza Bandari ya Wete Ndugu Bakhresa pindi akimaliza ujenzi wa bandari iweze kutumika kwa vyombo vyote vya majini kama ilivyo kwa bandari ya Malindi.

c) Kamati imeishauri Shirika la Bandari kufikiria wazo la kuweka kipaa katika bandari ya Mkoani.

MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

Mamlaka ya usafiri baharini ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya Baharini, sambamba na jukumu hilo la msingi mamlaka inasimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogovidogo, utaaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia pamoja kusimamia shughuli za upakiaji wa abiria kwa kushirikaana na taasisi nyengine, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yake ingawa bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali zinazokwamisha shughuli zao, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

CHANGAMOTO

1. Kuchelewa kwa Tanzania kuridhia Mkataba wa **"Maritime Labour Convention"** kunasababisha meli za Zanzibar kuzuiwa katika bandari za kigeni, kutokana na mabaharia wa meli hizo kutokuwa na vyeti vya ubora ambavyo mamlaka haiwezi kutoa vyeti hivyo kwa vile mkataba huo hauajridhiwa na nchi yetu.

2. Ukosefu wa jengo la Ofisi.: mamlaka ya usafiri baharini bado inaendelea kukabiliwa na changamoto ya kukosa jengo la ofisi hali ambayo inawalazimu kukodi jengo kwa gharama kubwa

3. Ukosefu wa vifaa vya uokozi: licha ya Mamlaka kuwa na jukumu la kusimamia usalama wa vyombo vya baharini ni ajabu kubwa kuwa inakosa vifaa kwa ajili ya kusimamia usalama huo ikiwa ni pamoja na vifaa vya uokozi na boti za ufuatiliaji hali inayozorotesha shughuli zao.

4. KUHUSU KUSITISHWA KWA MKATABA WA PHILTEX

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnamo mwaka wa 2007 ilfunga mkataba na kampuni ya Philtex Corporation (BELIZE) Limited kwa kazi za kuendesha uwakala wa kusajili Meli za kigeni kwa niaba ya Serikali mkataba ambao ulikuwa ni wa miaka 10. Madhumuni makubwa ya

Serikali kuanzisha Wakala huo ni kutoa fursa kwa Zanzibar kushiriki katika biashara ya kimataifa ya usafiri baharini na pia ni njia ya kujiongezea mapato kwa ajili ya uendeshaji kazi za usimamizi wa usalama wa usafiri Baharini.

UAMUZI WA KUSITISHA MKATABA WA KAMPUNI YA PHILTEX.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifikia uamuzi wa kusitisha mktaba na kampuni ya philtex mnamo mwezi wa Januari 2013 uamuzi ambao ulitokana na wakala huyo mara kadhaa kukiuka vikwazo vya kimataifa vilivyoekwa dhidi ya nchi ya Iran, pamoja na kuwa wakala huyo alitakiwa kuzifutia usajili meli 36 mnamo mwezi wa Julai 2012 na kutekeleza agizo hilo lakini bado alibainika kuendelea na kuzipatia usajili meli nyengine za Iran kinyume na agizo la Mamlaka ya usafiri la kutakiwa asite kusajili meli hizo.

Serikali ya Mapinduzi iliunda kamati ya kusimamia usitishaji wa Mkataba huo ambayo pamoja na mambo mengine ilikuwa na jukumu la kutafuta kampuni nyengine itakayoendesha biashara ya kusajili meli kwa niaba ya Serikali ambapo hatimae ilipatikana kampuni ya Al –Khaleej Industries iliyopo maeneo ya Bandari huru Sharjah ambayo kwa mujibu wa mkataba wake itakuwa na jukumu la kutafuta Ofisi (logistical Support) pamoja na kutafuta soko (Marketing Services) mkataba huo ulifungwa tarehe 11 Oktoba 2014.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI

a) Kuhusiana na kusitishwa kwa Mkataba wa Philtex na hatimae kufunga mkataba na Al-Khaleej kuendeleza kazi ya uwakala wa kusajili Meli, kamati inaishauri Serikali kufanya uchunguzi wa kina juu ya Kampuni hiyo ili kujua kampuni hiyo inamilikiwa na nani na historia yake kwa ujumla, ili kuepuka yale yaliyojitokeza kwa Kampuni ya Philtex.

b) Kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufuatilia na kuhakikisha kuwa Mkataba wa **'Maritime Labour Convention'** unaridhiwa haraka iwezekanavyo ili kuipa uwezo Mamlaka kutoa vyeti vya ubora kwa mabaharia wa Zanzibar.

c) Kamati inaishauri Wizara kulipa kipaumbele suala la kuwapatia jengo la Ofisi Mamlaka ya Usafiri Baharini katika Bajeti ya mwaka 2015/2016 ili waondokane na tatizo la kukodi jengo kwa gharama kubwa.

d) Kamati inaishauri Mamlaka ya Usafiri Baharini kutunga kanuni itakayoweka kiwango cha idadi ya watoto ambao mzazi mmoja ataruhusiwa kusafiri nao katika meli na boti za abiria.

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ina jukumu la kusimamia, kuendesha na kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Unguja na Pemba kwa kuzingatia miongozo na kanuni za kitaifa na kimataifa, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka imeendelea na shughuli zake kwa ufanisi ingawa bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali kama hizi zifuatazo:-

CHANGAMOTO

1. Mamlaka inakabiliwa na tatizo la uharibifu wa mazingira unaofanywa na wanachi hali inayowalazimu kukodi Kampuni ya ulinzi ambacho kinawaharimu shilingi milioni ishirini kwa mwezi kwa ajili ya malipo ya kikosi hicho.

2. Ufinyu wa Bajeti; mamlaka inakabiliwa na ufinyu wa bajeti hali inayopelekea kuzorota kwa shughuli za Mamlaka na ukizingatia mamlaka haina vyanzo vya kutosha vya kukusanya mapato

3. Kukosa mashirikiano mazuri kutoka katika taasisi ya Muungano ambayo ni TCAA katika utekelezaji wa kazi zao hasa pale Qatar Airways walipoomba kibali cha kuwachukua watalii kutoka Kilimanjaro na kuwaleta Zanzibar (ride to Carbotage) katika dhamira ya kukuza utalii Zanzibar lakini cha kusikitisha ni kuwa TCAA wamekataa maombi hayo.

4. Kuwepo kwa matatizo mengi yanayowakabili askari wa zimamoto katika uwanja wa ndege wa Pemba, ikiwemo ukosefu wa nguo maalum za kuzimia moto, eneo la kupumzikia, vifaa vya kuzimia moto, ambapo licha ya uongozi wa kiwanja kufikisha maombi katika Wizara husika lakini bado hakuna mabadiliko yoyote.

5. Kwa kuwa baada ya kukamilika kwa ujenzi na kuanza kazi ya uendeshaji wa Terminal II kutakuwa na mahitaji ya wafanyakazi wapya karibu 400 kwa Unguja na Pemba ambao watahitaji mafunzo na kufikiriwa masuala ya mishahara yao, bado suala hili halijafikiriwa na Wizara na kufanyiwa matayarisho yoyote.

6. Kukosekanakwa mashirikiano ya karibu baina ya Mamlaka na Wizara hasa katika miradi inayohusu uendelezaji wa viwanja vya ndege.

7. Baadhi ya Waheshimiwa ambao wanaingia uwanja wa ndege wanaleta usumbufu wakati wa kukaguliwa jambo ambalo ni muhimu kufanyika katika kulinda usalama wa maeneo ya viwanja.

MAPENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI

a) Kwa kuwa utalii ni miongoni mwa sekta muhimu ya uchumi kwa Zanzibar kamati imeiagiza Wizara ya miundombinu na Mawasiliano kulifuatilia suala la Qatar Airways kuruhusiwa kushusha watalii kutoka Kilimanjaro lililokwamishwa na TCAA ikizingatiwa kuwa taasisi hiyo ni ya Muungano.

b) Kamati inaishauri Wizara kuandaa mpango wa uajiri wa wafanyakazi wapya watakaohudumia Terminal II mapema ili kuja kuepusha mzigo kwa Mamlaka ya uwanja huo.

c) Kamati inaishauri Wizara kuwashirikisha kwa karibu zaidi Mamlaka ya Viwanja vya Ndege katika miradi inayohusu uendelezaji wa Viwanja vya ndege kwani wao watakuwa na utaalamu na uwelewa zaidi juu ya masuala yanayohusiana na viwanja hivyo.

d) Kamati inaishauri mamlaka kulichukua suala la kuwatengenezea mazingira mazuri askari wa kikosi cha zimamoto kwani Wizara inayohusika na vikosi hivyo inachelewa kulitekeleza jukumu hilo.

SEHEMU YA TATU

HITIMISHO

Katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya 1984 na kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, Toleo la mwaka 2012. Kamati imetoa maelekezo na ushauri mbali mbali ambao kamati unaamini utasaidia kutatua changamoto na kasoro tulizoziainisha kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya kuleta Maendeleo kwa Wananchi wa Zanzibar.

Kamati inatoa shukurani za dhati kwa watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupatia wakati wa utekelezaji wa kazi za Kamati. Aidha shukurani za pekee tunazitoa kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu na watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha kamati kwa hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.